## UMBO LA MTIHANI WA KITAIFA KISWAHILI

**(A) VIHASHO (Maswali 15)**

- Sehemu hii mara nyingi huwa na sehemu mbili zenye vihasho
- Sehemu ya kwanza huwa na vihasho kuanzia nambari ya kwanza hadi ya saba au nane
- Sehemu ya pili huviendeleza vihasho kuanzia nambari nane au tisa hadi kumi na tano

**MWONGOZO WA KUYAJIBU MASWALI KATIKA SEHEMU HII**

- Isome taarifa pamoja na vihasho juu juu ili uweze kuju au kukisia kinachozungumziwa, nyakati, vionyeshi, nomino na ngeli.
- Isome taarifa Kwa makini kisha ujaribu kuzijaza nafasi zilizo wazi kwa maneno yako mwenyewe.
- Ikiwa utashindwa, tazama mfumo wa viteuzi
- Tazama ikiwa wametumia visawe katika viteuzi.
- Yaandike majibu yako kwenye vihasho.
- Isome taarifa pamoja na majibu yako ikiwa ina mtiririko mwafaka wa visa au matukio.
- Yaandike majibu yako kwenye karatasi ya majibu.

Baadhi ya Vipengele vinavyotahiniwani kama vile:

- ✓ Sarufi
- ✓ Ngeli
- ✓ Viunganishi
- ✓ Vivumishi
- ✓ Virejeshi
- ✓ Vihusishi
- ✓ Vielezi
- ✓ Vitenzi
- ✓ Misamiati teule
- ✓ Vihisishi
- ✓ vishirikishi

**(B). MATUMIZI YA LUGHA (Maswali 15)**

Baadhi ya vipengele ambavyo hutahiniwa katika sehemu hiini kama vile.

**i) Kusikiliza na kuongea (Salamu, Semi, herufi, sauti, )**

***Herufi mwambatano***

Konsonanti (herufi) mwambatano zina herufi mbilimbili au tatu tatu

Herufi mwambatano zenye herufi mbili ni: *Ch, dh, gh, kh, mb, nd, ng, ng', ny, sh, th*

Herufi mwambatano zenye herufi tatutatu ni: Mbw, shw, ngw,njw, nyw,…….

Tanbihi: baadhi ya herufi hizi hazipatikani katika orodha ya alfabeti za Kiswahili

***Sauti changamano***

Herufi Mwambatano zikiambatanishwa na irabu zinakuwa "Sauti Changamano" Mifano: Onywera, Chama, Dhehebu, Mbuzi, Njiwa, Nyama, Nyongesa, Khalwale, Wanyonyi, Naliakha, Mwinyi, Abdallah

***Sauti Ghuna***

Ukizitamka herufi hizi ukiwa umeliziba sikio kwa vidole, masikio yanatoa mngurumo au kitetemeshi kooni au kwenye viwambo vya masikio.

*Mifano ya sauti ghuna ni:* **b, dh, d, g, j, m, n, ng', ny, v, z**

***Sauti sighuna***

Ukizitamka herufi hizi ukiwa umeliziba sikio kwa vidole, masikio *hayatoi* mngurumo au kitetemeshi kooni au kwenye viwambo vya masikio.

Mifano ya sauti sighuna ni: **f, h, k, p, s, t**

| | | |
|---|---|---|
| 2005 – 24 | 2011 – 18 na 24 | 2016 – 18,21, 26 &30 |
| 2007 – 26 na 28 | 2013 – 20, 24 na 29 | 2017 – 8, 17, 24 |
| 2008 – 30 | 2014 – 30 | 2018 - 16 |
| 2009 – 29 | 2015 – 21 na 27 | |

**ii) Sarufi**

a) Umoja na wingi wa sentensi / nomino

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2002 – 19 | 2007 - 18 | 2011 - 25 | 2014 - 18 | 2017 - 16 |
| 2004 – 17 | 2008 - 23 | 2012 -17 | 2015 – 18 | 2018 – 18,28,29 |
| 2005 - 29 | 2010 - 17 | 2013 – 19 | 2016 - 29 | |

b) Sentensi iliyo sahihi kisarufi au kimantiki

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2000 -19, 20, 23 | 2003 – 19 | 2006 - 17 | 2010 - 16 | 2018 – 19, 20 |
| 2001 – 27 na 30 | 2004 – 28 | 2008 - 27 | 2014 - 25 | |
| 2002 – 23 | 2005 – 27 | 2009 - 21 | 2016 - 16 | |

c) Matumizi ya viambishi ainati k.v.(KI, KWA, NA, PINDI, KA, WA,JI, LAU, NA, NI ...........)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2000 – 16 | 2004 – 19, 29 | 2008 - 17 | 2012 –27 | 2017 - 26 |
| 2001- 29 | 2005 – 22 na 28 | 2009 - 16 na 20 | 2013 – 17 na 23 | 2018 - 22 |
| 2003 – 23 | 2006 – 16 | 2011 – 17 na 21 | 2015 - 28 | |

d) Ukubwa na udogo

2000 – 22 2002 – 29 2003 – 21 2013 - 3

e) Kukanusha

| | | |
|---|---|---|
| 2001- 21 | 2012 - 24 | 2017 - 20 |
| 2005- 18 | 2014 - 16 | 2018 - 24 |
| 2009- 17 | 2015 - 25 | |

f) Jinabaki au Uingiliano

| | | |
|---|---|---|
| 2003- 27 na 28 | 2010-21 na 24 | 2015 - 20 |
| 2005 -17, 26 na 30 | 2011-22 | 2017 - 25 |
| 2006 - 27 | 2013 – 28 | |

g) Mpangilio wa maneno katika kamusi

2001 – 22 2012 - 16

2006 - 30 2015 - 16

h) Uti wa mgongo wa Kiswahili( Ngeli, Nomino, Vivumishi, Vielezi, Vihisishi, Vitenzi, Viunganishi na Viwakilishi)

| | | |
|---|---|---|
| 2000 – 19,21, 26 na 27 | 2007– 17, 19, 20, 21, 25 | 2014 – 20, 23 |
| 2001 – 18,24 na 28 | 2008-24 na 28 | 2015 – 19, 22, 23, 24, 30 |
| 2002 -20 na 22 | 2009– 22 | 2016 – 19, 20, 25, 28 |
| 2003 – 16, 22 na 30 | 2010- 18, 19, 20 na 27 | 2017 – 18, 21, 23, 27, 30 |
| 2004– 20, 23, 25, 26, 27,30 | 2011– 16, 20 na 28 | 2018 – 17,21, 30 |
| 2005– 20 na 21 | 2012– 18, 26, 28 na 29 | |
| 2006– 19, 22, 23 na 26 | 2013– 16, 21 na 22 | |

i) Usemi halisi na wa taarifa

| | | |
|---|---|---|
| 2001 - 23 | 2008 - 16 | 2014 - 17 |
| 2004 - 22 | 2009 – 19 | 2016 – 22 |
| 2005- 19 | 2010 - 28 | 2017 -22 |
| 2006 - 29 | 2013 – 18 | 2018 - 25 |

j) Kinyume 2008 – 19 2012 21
k) Uakifishaji 2015 – 17 2017 – 29 2018 – 23

**iii ) Misamiati**

| | | |
|---|---|---|
| 2000 - 28 | 2007 –16, 24, 27 na 30 | 2014 -19, 21, 23, 24, 26, 27, 28, 29 |
| 2001 – 16, 17, 19, 25 na 26 | 2008 – 18, 22, 26 na 29 | 2015–26 & 29 |
| 2002 – 18, 25, 27 na 30 | 2009 – 18 na 23 | 2016 – 17, 24 na 27 |
| 2003 – 18, 24, 25 na 26 | 2010 – 23, 24, 25 na 26 | 2017 – 19, 28 |
| 2004 – 21 | 2011 – 30 | 2018 – 26, 27 |
| 2005 – 16 na 23 | 2012 – 19, 20, 22, 23 25 na 29 | |
| 2006 – 18,24, 25na 28 | 2013 – 25, 26 na 27 | |

**UFAHAMU;**
Kuna ama mbili za ufahamu: Ufahamu *halisia* na ufahamu *simulizi*
**Mwongozo wa kuyajibu maswali:**
- Isome taarifa juu juu ili ujue yanayozungmziwa
- Isome taarifa kwa makini msitari baada ya mwingine ili ukisie, uone, uguse na ubuni yanayosimuliwa.
- Yasome maswali yote Kwa makini ukiwa na taarifa kichwani
- Ipatie mistari ya ufahamu nambari mwanzoni mwa aya.
- Rudi kwenye maswali ukiwa na taarifa kichwani ili uitambue misitari / sehemu zinazolijibu kila swali
- Isome sehemu/ aya uliyoitambua kuwa inalijibu swali husika
- Yadondoe majibu mawili ambayo ni duni
- Chagua jibu sahihi kati ya viteuzi viwili viliyobaki.

**Tahadhari**: Maswali yanayohusu Kichwa mwafaka au methali inayofaa yatahitaji matumizi ya wazo au funzo kuu kutokana na taarifa au habari.

**UANDISHI WA INSHA**
- Insha ni sehemu muhimu katika karatasi ya Kiswahili
- Katika kuiandika insha, mtahiniwa huhitajika kuuonyesha uwezo na umahiri wake wa **kubuni** na kuitumia lugha ya Kiswahili **kwa mnato wa aina yake**
- Katika ule utunzi, mwandishi anahitajika kuyateua maneno yaliyo na mnato na mvutio wa kipekee ili autoe ***MTUNGO***.

**Mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa insha**

i. **Maagizo** - Maagizo yatampatia mwandishi mtindo unaohitajika
- Kuna mitindo mbalimbali inayoweza kujitokeza kulingana na swali husika kama vile:
  - ✓ Masimulizi –Anzilishi au ishilizi
  - ✓ Hotuba
  - ✓ Methali
  - ✓ Barua (Kirafiki na Rasmi)
  - ✓ Kumbukumbu

ii. **Muda** – Mwandishi atahitajika kuutumia muda wake vizuri ifuatavyo
Dakika **5**-Kuandika vidokezi- Viwe vitakavyokupa urefu unaohitajika
Dakika **30** –Kuiandika insha yenyewe
Dakika **5** – Kuipitia insha

iii. **Vidokezi** – Itambidi mtahiniwa aviandike vidokezi ili vimwongoze katika uandishi wake. Vidokezi hivi vitampatia mwandishi mada mwafaka

iv. **Utangulizi** –Mwandishi atahitajika kuutanguliza mtungo wake kwa kishindo ili kumteka mtahini na aweze kuzama katika insha

v. **Maudhui**(Alama 20) – Hiki ni kipengele muhimu. Mwandishi atahitajika kuyajibu maswali yafuatayo:

- ✓ Lini?
- ✓ Wapi ?
- ✓ Nani?
- ✓ Vipi?
- ✓ Kwa nini

vi. **Msamiati** (Alama 12) – Msamiati si mabonge wala mabonbwe ya maneno.Uteuzi mwafaka wa msamiati utategemea mazingira ya mwandishi.

vii. **Mtindo au Mwundo** (Alama 5) – Mpango utategemea swali na maagizokutok kwa mtahini. Mwanafunzi hana budi kuyafuata maagizo ipasavyo ili asipoteze alama tatu muhimu.
Mtahiniwa ahakikishe amepanga aya zake vizuri

viii. **Mtiririko na mshikamano** (Alama 3) - Mtiririko mwafaka utaonekana ikiwa mwandishi atazingatia mtiririko wa vidokezi kutoka **Mwanzo-Mwili-Tamati**

ix. **Sarufi na Tahajia** – Dakika tano za mwisho zitumiwe kuipitia insha ili kuyarekebisha makosa ya hijai na tahania kama vile:

- ✓ Maendelezo mwafaka wa maneno
- ✓ Sarufi

x. **Hati** – Hati nzuri humpatia mtahini kazi rahisi wakati wa kuisahihisha insha ya mtahiniwa. Mwanafunzi atahitajika kuandika kwa mwandiko unaosomeka kwa urahisi.

xi. **Ubunifu na uteuzi wa maneno** - Mtahiniwa huhitajika kutafuta nja na mbinu za kumfanya mtahini atamani mtungo usiishe. Katika hali hii, mtahini huhitajika kuufanya mtungo wake uwe wa kuvutia kwa kutumia fani ainati za lugha k.v:

xii. **Tahakiki**–Ni maneno yanayotumia msamiati teule ulio na uzito, utamu na mnato wa aina yake. Baadhi ya tahakiki hizi ni kama vile za kuamka, furaha, harusi, umaskini n.k. Baadhi ya mifano ni kama vile:

- ✓ Niliamka subuhi kabla ya bwana shamshi kupasua matlahi……..
- ✓ Kuche kusiche, hatimaye kulikucha ………
- ✓ Ukumbi ulijaa shangwe, nderemo, vigelelgele, vifijo, chereko na kayaya za adani kwa ndani
- ✓ Maskini wa kula kwa haidhuri na kuamka kwa afadhali

xiii. **Methali**- Methali itategemea wazo katika aya

xiv. **Vitanasifa** – Sifa zinazosisitiza kuhusu nomino fulani

- ✓ Mrefu njorinjori
- ✓ Bibi arusi alikuwa mrembo kichunechune
- ✓ Ndugu halisa
- ✓ Mzima hadidi
- ✓ Mnene tibwatibwa/ Tipwatipwa

xv. **Istiara** – Hali ya kulinganisha moja kwa moja k.v

xvi. **Tashbihi / Tashbiha**- Kulinganisha kwa kutumia kama, mithili ya,ja

xvii. **Chuku(Matilia chunvi)** – Hali ya kusema uongo ulio na mipaka k.v.

- ✓ Ukumbi ulijaa kiasi cha kuwatapika wengine nje
- ✓ Tulibanana kama ndizi
- ✓ Mweusi pi kiasi chakuyafanya makaa yamwonee wivu/gere

xviii. **Tabaini** - Hali ya kutumia maneno yanayogongana ili kuleta msisitizo kwa kutumia **SI au HA**

xix. **Tashdidi** – hali ya kutumia maneno yanayokaribiana kimaana ili maana ya ujumbe ijitokeze waziwazi k.v:

- ✓ Nilimpenda na kumwenzi
- ✓ Tambua na ng'amua
- ✓ Fika na kuwasili
- ✓ Amka na kudamka
- ✓ Tazama na kumwona

xx. **Nahau** – hali ya kutumia amneno yenye maana isiyotokana na maana ya kawaida za maneno hayo k.v:

- ✓ Kunja jamvi
- ✓ Tupa jongoo na mti wake
- ✓ Piga maji

xxi. **Majazi** - hali ya kuwapa wahusika majina kulingana na sifa zao k.v domo Kaya, Upendo, malkia, Boramimi, Simimi n.k

xxii. **Balagha** – Fani ya kutumia maswali yasiyohitaji majibu katika mtungo

xxiii. **Tanakali za sauti** –Chinja twaa.mulika mwaa, nuka fee

xxiv. **Nomino za makundi**- Kama vile: Kilinge cha askari,rubaa la watafiti, fara la pishi, mpwito wa furaha

xxv. **Nomino za kiasi** – Mifano ni kama vile: Tonge la ugali, Udole wa ndizi, Gunzi la mahindi, Finyu la tumbaku

xxvi. **Shada** – hali ya uradidi wa maneno ili kuleta usemi Fulani il kuleta maana ifaayo.Mifano ni kama vile:

- ✓ \Bure bilashi
- ✓ Kutia na kutoa
- ✓ Sina uhusiano naye wa damu wala usaha

xxvii. **Taswira jozi** – Mafungu ya maneno mawili yanayotumiwa sambamaba ili kuleta msisitizo mwafaka k.v.

- ✓ Kiko na digali
- ✓ Bega kwa bega
- ✓ Alfajiri na mapema
- ✓ Tende na halua

xxviii. **Nomino jozi** – Haya ni maneno yanayotumika jozi jozi kama vile

- ✓ Wahenga na wahenguzi
- ✓ Waganga na waganguzi

xxix. **Tasfida** –Matumizi ya maneno yanayoonyesha adabu na heshima

*"TAFADHALI USIANDIKE, TUNGA*

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA INSHA**

- Kuna vipengele vitano vinavyozingatiwa na watahini wakati wa kusahihisha mitungo.

**(a) MAUDHUI**: Ni hoja au mambo yanayozungumziwa, kuelezea au kuhadithiwa kuhusiana na mada mbalimbali mtahiniwa alizopewa ili kuandikia insha. Katika kipengele hiki cha maudhui mtahiniwa anatarajiwa **kutunga au kubuni** kisa na kukifafanua kwa kina ili kuudhihirisha uwezo wake wa ubunifu.

- Katika kipengele chenyewe ndipo ambapo mtahini ataweza kujua kama yaliyomo ni kazi asilia ya mtahiniwa na kuamua inavyopasa kama uwezo wa ubunifu wa yule mtahiniwa ni wa **juu ya wastani,wastani, chini ya wastani** au **amepotoka** kabisa kwa kuandika jambo lolote kuhusiana na kila mada mojawapo. Ni vizuri kufahamu kuwa mtahiniwa yeyote kunukuu au kunakili tu insha zilizotungwa na watu wengine na kudai ya kwamba ametunga insha ni kujidanganya tu.
- Yafaa kufahamu kinagaubaga ya kwamba katika swali la utungaji wa insha,.uwezo wa ubunifu wa mtahiniwa binafsi ndilo jambo hasa linalotahiniwa. **Alama za juu kabisa zituzwazo kwenye kipengele hiki cha maudhui ni 20.**

Kwa maana hii basi, kabla ya mtahini kuufikia uamuzi wake juu ya alama atakazotuza kwenye kipengele hiki cha maudhui, atafaa ajiulize na kuzingatia maswali yafuatayo: -

Je, yale mambo ambayo mtahiniwa alitarajiwa kuzungumzia, kuelezea au kuhadithia katika insha yake:

i) Ameridhisha kwayo?

ii) Ameyatoa kwa wastani au kwa uchache sana?

iii) Amepotoka kabisa?

**TANBIHI:** Kabla ya kutuza alama za kipengele hiki mtahini aurejelee mwongozo dira

**b) MSAMIATI NA MATUMIZI YAKE**

- Msamiati ni jumla ya maneno yote katika lugha husika.Msamiati hutumiwa na mwandishi ili kutunga na kuunda sentensi akitumia miundo mbalimbali ya sentensi kwa nia ya kuuwasilisha ujumbe wake kwa msomaji wa kazi.
- Hivyo basi, yampasa yule mtahiniwa azingatie vizuri sarufi safi pamoja na kuyaendeleza maneno kwa usahihi huku akitia katika insha yake madoido kwa kutumia fani mbali mbali za lugha mathalan methali, nahau, istiara, vielezi vya misemo sisitizi (k.m tulia tuli, lewa chopi, giza totoro, kiguu na njia, juu chini, pata shika n.k) katika lugha ili kujenga au kutoa kwa ukamilifu taswira ya jambo au mamboanayoyaeleza katika insha yake.

  Kutokana na msamiati alioutumia pamoja na miundo mbalimbali ya sentensi na jinsi alivyojitahidi kuisarifu lugha kwa jumla, mtahini ataweza kujua na kuamua inavyostahiki ikiwa mtahiniwa yule anaimudu lugha kwa kiwango cha juu ya wastani, wastani au chini ya wastani.Alama za juu kabisa zituzwazo kwenye kipengele hiki cha msamiati ni 12

  Mtahini atatakiwa ajiulize maswali yafuatayo:
- Je, uteuzi wake wa msamiati wa insha alioutumia katika insha yake katika kuuwasilisha ujumbe wake waridhisha? Yaani ametumia katika insha yake msamiati wa hali ya juu na ambao haujapachikwapachikwa ovyo ovyo tu bali ameambatana vizuri na yale mambo anayoyazungumzia?
- Je, msamiati alioutumia katika insha yake ni wa juu ya wastani, wastani au chini ya wastani?
- Je, ametumia kwa usahihi katika insha yake baadhi ya tamathali za lugha kamam vile misemo, tashbihi, vielezi vya mkazo na misisitizo mingine katika lugha ama ameyapachikapachika baadhi ya mambo yale ovyo ovyo tu katika insha yake?
- Je, amezingatia sarufi safi wakati wa kutunga au kuunda sentensi zake pamoja na kuyaendeleza maneno kwa usahihi au mambo yale ameyavuruga kwa kiasi Fulani?
- Utuzi wa alama:
- Uteuzi mwafaka wa msamiati kulingana na mada - alama 4
- Kiwango cha msamiati uliotumika vizuri pasi kupachikwapachikwa ovyoovyo – alama 6
- Matumizi ya msamiati kwa kutumia sheria / kanuni za sarufi – alama 2

**(c) MTINDO NA MUUNDO** -Muundo ni utaratibu wa kufanyia jambo hatua kwa hatua na kwa mpangilio mzuri tena wa kuvutia.Tunayo mitindo mbalimbali ya kuhadithia visa, kadhia au mambo mbalimbali kama vile ushairi, barua, hadithi, kumbukumbu za mikutano n.k.

- Kila mtahiniwa atafaa kutumia mtindo mwafaka kulingana na mada aliyopewa. Muundo ni mkao wa vitu au jinsi linavyoonekana.Muundo hujumulisha sura,mpangilio wa kazi kiaya, hati na usafi. **Alama zajuu kabisa zituzwazo kipengele hiki cha mtindo au muundo ni tano (5)**
- Mtahini atahitajika kujiuliza maswali yafuatayo kabla ya kumtuza mtahiniwa:
- Je, mpangilio wa mambo katika insha yake waridhisha au ameyaparanganya maelezo kiasi cha kutoeleweka?
- Je, wakati wa kuiandika insha yake ametumia mtindo mwafaka kulingana na mada aliyopewa kuandikia?
- Je, aya au ibara katika insha zake zimepangwa kwa njia ya kuvutia?
- Je, insha yote kwa jumla inavutia jinsi ilivyoandikwa?

**(e) MTIRIRIKO NA MSHIKAMANO**

- Huu ni mfuatano mzuri wa mawazo kutoka sentensi moja hadi nyingine, aya moja hadi nyingine na katika insha yote kwa jumla.Mshikamano ni mwambatano mzuri wa mawazo kuanzia mwanzo hadi mwisho wa insha.**Alama za juu kabisa zituzwazo kipengele hiki cha mtiririko na mshikamano ni tatu (3)**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Maudhui (Ma)________________ | 20 |
| ii. | Msamiati (Ms)________________ | 12 |
| iii. | Mtindo na Muundo(Mt/Md)__________ | 05 |
| iv. | Mtiririko na mshikimano(Mtr/Msh)_____ | 03 |
| | JUMLA____________________ | 40 |